Nipashe Uk.1 Mei 26,2021

# YALIYOMO

UKURASA WA 4

## WAFUGAJI KUTOLEWA HIFADHINI KWA OPERESHENI

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk.Damas Ndumbaro, ametangaza operesheni ya kuwaondoa...

Scanned with CamScanner

Daily News pg.16 May 26,2021

# Plans to curb illegal fishing nets in pipeline

**By DAILY NEWS Reporter**

THE government is working on a mechanism to identify fishing nets manufacturing process and distribution to fishermen to control illegal nets in the country.

This was revealed in Mwanza Region yesterday by the Deputy Minister of Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega during his meeting with Kanyala Village residents in Sengerema District.

"We are well prepared to monitor manufacturers who produce and bring to the market outlawed fishing nets. Fishermen in the country have been in dilemma for quite some time as when they procure such nets, they end up being in trouble while no measures are taken to manufacturers and distributors," he said

Mr Ulega said to ensure that fishing nets meet the required standards; the ministry in collaboration with the Tanzania Bureau of Standards (TBS) will establish a system that will be nationally recognized to save fishermen from further incurring a loss.

The deputy minister also commended the residents of Kanyala Village in Sengerema District for showing a broad understanding of the non-use of illegal fishing gears in collaboration with the government which has significantly reduced illegal fishing activities.

Regarding the establishment of fishermen cooperatives, he said the government plans to enable fishermen through these associations to obtain loans so that they can purchase more modern fishing equipment.

In ensuring that fishermen's cooperatives benefit from loans through various financial institutions including the Tanzania Agricultural Development Bank (TADB), Mr Ulega has urged associations that have already received loans to make timely repayments so that they can qualify for further lending as well as facilitate other parties to get loans and promote the fishing industry.

For his part, Buchosa Member of Parliament, Eric Shigongo commended the Ministry for ensuring that it manages the interests of fishermen and called on them to control illegal fishing nets before they reach the fishermen, by inspecting nets from people or companies licensed to import the nets.

The Sengerema District Commissioner, Mr Emmanuel Kipole also rebuked corrupt practices and urged fishermen not to give bribes to any government official as by doing so they are justifying the continued existence of such acts.

He called on the authorities involved in the seizure of illegal fishing gear to comply with the country's laws as corrupt practices destroy the country and lead to a lack of good relations between the operators and the fishermen.

Some residents of Kanyala Village, speaking at a meeting with the Deputy Minister, have complained about some fishermen's cooperatives lacking loans from various financial institutions despite following the procedures that have been linked to those institutions.

Scanned with CamScanner

# China boosts VETA in fishing courses

**By HILDA MHAGAMA**

THE Chinese government yesterday donated fishing and fish processing tools worth 350m/- to Vocational Education and Training Authority (VETA).

The donated equipment includes a fishing boat, boat making and maintenance tools and mincing as well as grinding gears.

Speaking during the handover ceremony in Dar es Salaam, Minister for Education, Science and Technology, Prof Joyce Ndalichako said the donation follows a commitment made by the Chinese Foreign Minister Wang Yi, who was in Chato on January 6, 2021, during the inauguration ceremony of VETA Training Centre.

Prof Ndalichako said the VETA Centre in Chato is the first vocational training in the country to offer fishing and fish processing courses, thus [illegible] support is very import[illegible] [illegible]tablishing those noble courses for occupation in the fishing related sector.

"On behalf of the government, I would like to convey my sincere appreciation to the government of China for continued support to Tanzania, especially in the education and vocational skills sector that has supported the production of skilled and competent labour force," she said.

Earlier, Chinese Ambassador to Tanzania, Wang Ke, said the donation also demonstrates the friendship between the Chinese people and Tanzania and the sincere support of China to education in Tanzania.

"For any country, particularly the developing countries, education constitutes the foundation of the country and human resources, which are the first productivity, thus our two countries attached very much importance in education," she said

According to her, China has been providing funds in various educational establishments in Tanzania, where they also provide scholarships annually to more than 100 Tanzanians. Over the past three years, the Chinese government under 'Rafiki Programme has provided all together 1.1bn/- to support various education projects in 12 regions in Tanzania.

Currently, there are 712 vocational training colleges across the country, up from 672 that were recorded in 2015, and 62 of them are owned by the government. Out of the 62 colleges, 20 serve the regional level, while the remaining 42 are at the district level

VETA Board Chairman, Mr Peter Maduki said they aim at improving and expanding vocational training in Tanzania.

"The government is currently constructing 33 VETA centres, among which four are regional and 29 at district levels," he said

Daily News pg. 2, May 26,2021

Scanned with CamScanner

Daily News pg. 1, Mei 26,2021

# Dar, Riyadh seek to bolster ties

By DEOGRATIUS KAMAGI

PRESIDENT Samia Suluhu Hassan has invited Saud Arabia to strengthen the cooperation with Tanzania by exploring business and investment opportunities available in the country.

President Samia specifically mentioned trade opportunities on livestock, fisheries and agricultural products that are abundant in Tanzania.

The Head of State was talking to Saudi Arabian Minister for Foreign Affairs Prince Faisal bin Farhan Al Saud, who paid a courtesy call on the president at the Dar es Salaam State House.

According to the statement issued by the Director of Presidential Communications, Mr Gerson Msigwa, President Samia also asked Saudi Arabia to open its consulate in Zanzibar.

**President Samia specifically mentioned trade opportunities on livestock, fisheries and agricultural products that are abundant in Tanzania.**

**Prince Faisal motioned the importance of maintaining the bond of the business persons from the two sides given the fact that there are direct flights connecting the two countries.**

The president also extended appreciation to the government of Saudi Arabia for its continued support towards improving water, infrastructure, education and health sectors in the country.

"Tanzania is ready to continue maintaining the existing relationship with Saudi Arabia for the sake of improving the economy and social welfare,"

Continues on Page 3

Scanned with CamScanner

# Operesheni sasa yaja kuwaondoa wafugaji hifadhini

**Na Gideon Mwakanosya,** TUNDURU

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk.Damas Ndumbaro, ametangaza operesheni ya kuwaondoa wafugaji waliovamia katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na maeneo mbalimbali yaliyotengwa kwa ajili ya utalii hapa nchini.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi wa vijiji vya Kalulu na Jakika wilayani Tunduru, alipofanya ziara ya kusikiliza kero zao kuhusiana na wanyamapori wanaovamia mashamba na kufanya uharibifu wa mazao wilayani humo.

Dk. Ndumbaro alisema tatizo la wanyama hususani tembo wanaokula mazao ya wakulima limechangiwa na wafugaji kuingiza mifugo yao kwenye maeneo yasioruhusiwa kisheria, jambo linalosababisha wanyama hao kukimbia.

Kwa mujibu wa Dk. Ndumbaro, serikali imeshatenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za ufugaji, lakini kutokana na kiburi cha fedha wafugaji wanawatumia baadhi ya wenyeviti na watendaji wa serikali za vijiji wasiokuwa waaminifu kukahidi na kupeleka mifugo.

Aidha, Dk. Ndumbaro aliwaonya wenyeviti na watendaji wa vijiji hao kujiepusha na vitendo vya rushwa kwa kupokea fedha na kuruhusu wafugaji kufanya shughuli zao kwenye maeneo ya utalii, kwamba tabia hiyo ni kukiuka sheria za utumishi wa umma.

Vilevile, Waziri Ndumbaro, aliwataka wananchi kuepuka kuishi, kufanya shughuli kwenye hifadhi, kwamba serikali haitahusika kulipa fidia wala kutoa kifuta machozi kwa mtu atakayepoteza maisha, kujeruhiwa na kuharibiwa mazao.

Nipashe Uk.4 Mei 26,2021

Scanned with CamScanner

Nipashe Uk.8 Mei 26,2

# SUA yaagizwa utafiti kubuni teknolojia kilimo cha kisasa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amekiagiza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kufanya utafiti wa kubuni teknolojia rahisi za gharama nafuu zitakazosaidia wakulima kuondokana na jembe la mkono ili kuleta uwiano mzuri wa matumizi ya teknolojia na kuongeza uzalishaji.

Alisema kwa kufanya hivyo watakuwa wamemuenzi kivitendo fikra za Hayati Edward Moringe Sokoine, ambaye alikipigania kwa nguvu zake chuo hicho ili kiweze kukuza uchumi wa wakulima na wafugaji kwa kutumia malighafi wanazozalisha.

Alisema hayo katika hotuba ya ufunguzi wa maadhimisho ya kumbukizi ya 17 la Chuo Kikuu SUA, kwa Hayati Sokoine ambaye alikuwa Waziri Mkuu, kiongozi mahiri na shupavu wa nchi ikiwa ni miaka 37 tangu kifo chake, Aprili 12, 1984.

Waziri Ndaki alisema matumizi ya teknolojia ya kisasa kwenye kilimo na ufugaji yana faida nyingi ikiwamo uzalishaji wa chakula cha kutosha, kuongeza kipato cha mkulima na mfugaji na kuchangia kupunguza umaskini. Alisema kuwa takwimu zinaonyesha asilimia 64 ya wakulima nchini wanatumia kilimo cha jembe la mkono ambacho tija yake ni ndogo.

Kadhalika, alisema sekta ya kilimo ndio msingi muhimu wa uchumi wa Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingine zinazotegemea kilimo kwa sababu kitaendelea kuwa na mchango mkubwa kwa uchumi kwa miaka mingi ijayo.

Waziri Ndaki pia alisema ukuaji wa sekta ya kilimo nchini kwa maana ya mazao ya kilimo, mifugo, misitu na uvuvi umekuwa haiendi kwa kasi inayotarajiwa kutokana na matumizi duni ya teknolojia.

Scanned with CamScanner

# Wizara: Leteni teknolojia tuache jembe la mkono

**Na John Nditi, Morogoro**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amezitaka taasisi za kitaaluma na utafiti kikiwemo Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) zibuni teknolojia rahisi na za gharama nafuu kuwezesha wakulima waache kulima kwa jembe la mkono na ufugaji wa mazoea.

Ndaki alisema hayo jana wakati akifungua maadhimisho ya kumbukizi ya 17 ya SUA kwa ajili ya Waziri Mkuu wa zamani, Edward Sokoine aliyekufa kwa ajali gari Aprili 12,1984 wakati akiwa njiani kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam.

Ndaki alisema matumizi ya teknolojia ya kisasa kwenye kilimo na ufugaji yana faida nyingi ukiwemo uzalishaji wa chakula cha kutosha, kuongeza kipato cha mkulima na mfugaji na hivyo kuchangia kupunguza umasikini.

Alitaja matumizi mengine kuwa ni uhakika wa masoko ya ndani na nje kutokana na wingi na ubora wa bidhaa zenye ushindani sokoni, upatikanaji wa malighafi za viwandani kwa ajili ya usindikaji na uzalishaji wa bidhaa kwa matumizi ya ndani na nje ya nchi.

Ndaki alisema sekta ya kilimo bado ni msingi muhimu wa uchumi wa Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingine zinazotegemea kilimo kwa sababu kitaendelea kuwa na mchango mkubwa kwa uchumi kwa miaka mingi ijayo.

Alisema uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, misitu na uvuvi hauendi kwa kasi inayotarajiwa kutokana na matumizi duni ya teknolojia.

Ndaki alisema takwimu zinaonesha kuwa asilimia 64 ya wakulima nchini hutumia jembe la mkono, asilimia 24 hutumia wanyamakazi na asilimia 12 tu wanatumia matrekta.

Alisema nchi pia haijafanya vizuri kwenye mifugo kwa kuwa kwa mujibu wa uchambuzi wa mwelekeo wa sekta hiyo Tanzania mwaka 2016/2017- 20231/2032 katika mwaka wa fedha 2019/2020 nchi ilizalisha lita bilioni 3.0 za maziwa.

Makamu Mkuu wa SUA, Profesa Raphael Chibunda alisema katika kutekeleza majukumu makuu ya kufundisha, utafiti na ugani, kimekuwa kikifanya vizuri kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi.

Profesa Chibunda alisema katika kutekeleza jukumu la utafiti SUA imekuwa ikifanya vizuri kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ambao ndio chanzo kikuu cha fedha za utafiti.

Alisema watafiti wao hupata wastani wa miradi ya utafiti 120 yenye wastani wa thamani ya Sh bilioni 25 kwa mwaka .

Habari Leo Uk.3 Mei 26,2021

Scanned with CamScanner

# JUKWAA LA UCHUMI



**MATARAJIO YA WANANCHI...**

WIZARA ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeendeleza kazi ya kugawa ardhi kwa...

UK.12

# Jinsi takwimu zinavyochangia ukuwaji sekta za kilimo, mifugo

Na WARIOBA IGOMBE

TANZANIA imeendelea kuandaa mipango, inayolenga kuimarisha uchumi na kupunguza umaskini.

Utekelezaji wa mipango hiyo, umeongeza mahitaji ya takwimu kwa lengo la kufuatilia na kupima mafanikio yanayopatikana.

Kati ya mambo muhimu yaliyopangwa kufanyika katika programu za kuimarisha uchumi na kupunguza umaskini, ni sensa ya kilimo, mifugo, uvuvi ili kupima mafanikio na kuimarisha uchumi wa kipato cha kati unaotegemea viwanda.

Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi(CCM) ya mwaka2020-2025, sura ya kwanza inaielekeza serikali,kuleta mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwa na uhakika wa chakula na kujitegemea kikamilifu.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), inasema takwimu za sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi zilizokusanywa katika sensa ya mwaka jana, zitatumika kupima na kutathmini utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kuendeleza sekta hizo.

"Takwimu hizo mbali ya kuonesha tulikotoka, tuko wapi, zitatuonesha kule tunakokwenda kutimiza malengo ya nchi kuimarisha kilimo, mifugo na uvuvi," anafafanua Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dkt. Albina Chuwa,alipokuwa mkoani Singida kukagua kazi ya ukusanyaji wa takwimu hizo.

Anasema kwa mara ya kwanza, sensa imefanyika kwa kutumia fursa zinazotokana na maendeleo ya teknolojia hasa ile ya digitali, ambayo imeboresha usahihi wa takwimu na kupunguza gharama ya kuzikusanya.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dkt. Anjelina Lutambi, anasema sensa ya takwimu ni kitu muhimu.

"Inatuwezesha tathimini kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa,takwimu sahihi zilizokusanywa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi imesaidia nchi kuwa kuingia kundi la nchi za uchumi wa kati,"anasema.

Dkt.Anjelina anasema , sensa iliyofanyika kwa lengo la kupata taarifa muhimu za kilimo, mifugo na uvuvi zitakazotumika kupanga na kutathmini utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya hizo nchini.

"Ukusanywaji huu takwimu, ukiwa katika ubora unaostahili, utasaidia kulifanya taifa kuingia uchumi wa juu, katika kipindi kifupi kijacho,"anasema.

Anasema taarifa za magonjwa ya mifugo na mazao, zitasaidia serikali kuainisha maeneo yanayokabiliwa na magonjwa, ili kuchukua hatua stahiki na kupanga mipango ya kudhibiti.

"Taarifa ya uzalishaji wa mazao zitasaidia kujua kiasi cha uzalishaji, kwa maeneo husika na kuiwezesha serikali kupanga upatikanaji wa masoko na uwezekano wa kuanzisha viwanda vya kusindika,mazao hayo,"anasema.





KATIBU Tawala mkoa wa Singida Dkt Anjelina Lutambi (aliyesimama)akizungumza katika mkutano wa uelimishaji kuhusu ukusanyaji takwimu za mifugo,kilimo na uvuvi katika Kijiji Msikii mkoani Singida.

Dkt.Anjelina anasema, taarifa ya upatikanaji na matumizi ya ardhi, zitatumika kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi na kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali Dkt.Chuwa, anasema matokeo ya sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi yanatarajiwa kuweka misingi imara katika sekta hizo.

> **Sekta ya kilimo ilichangia asilimia 24.3 ya mapato ya mauzo nje ya nchi mwaka 2019. Fedha hizi kwa kiasi kikubwa zinatumika katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, maji, usambazaji umeme na kuimarisha sekta za afya na elimu ili kuimarisha maendeleo ya wananchi,"**
>
> Naibu Waziri wa Kilimo Hussein Bashe.

Anasema sekta ya kilimo ina umuhimu katika mustakabali wa maisha ya binadamu, kwa kuwa ndiyo chanzo cha chakula na malighafi zinazohitajika viwandani.

Kupitia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya 2015- 2030, sekta ya kilimo ilipewa lengo la pili la kutokomeza njaa, kuwa na uhakika wa chakula, lishe bora na kukuza kilimo endelevu" anasema.

Anasema lengo hilo limesisitiza uwepo wa tija katika sekta ya kilimo, kwa kuongeza thamani ya mazao, kusisitiza matumizi bora ya ardhi na kurutubisha udongo, ili kuongeza mauzo wa binadamu kukabiliana na kuhimilimabadiliko ya tabia ya nchi, ikiwemo majanga mbalimbali kama mafuriko na ukame na majanga mengine ikiwemo ndege waharibifu.

Anasema sense katika sekta hizo, zitaleta tija kwa mtu mmoja mmoja kutatua changamoto hasa za upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani, upatikanaji wa masoko kwa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

"Ni muhimu tukafahamu takwimu sahihi za mifugo, mazao na uvuvi zitasaidia uchangiaji wa malighafi za viwanda vyetu hatua itakayochangia kukuza uchumi wetu," amesisitiza Dk. Anjelina.

Naibu Waziri wa Kilimo Hussein Bashe, akizungumza hivi karibuni katika mafunzo ya wadadisi wa sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi ya mwaka wa kilimo 2019/20, iliyofanyika Mwanza Julai, 25 mwaka jana, alisema Benki ya Dunia (WB) ilitangazaTanzania, kuwa katika kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati.

Anasema taarifa hizo zimeleta faraja kwa sekta ya kilimo, kwa kuwa ndiyo iliyotoa mchango mkubwa katika pato la taifa kwa asilimia 26.6 na ajira kwa takribani asilimia 66.

"Sekta ya kilimo ilichangia asilimia 24.3 ya mapato ya mauzo nje ya nchi mwaka 2019. Fedha hizi kwa kiasi kikubwa zinatumika katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, maji, usambazaji umeme na kuimarisha sekta za afya na elimu ili kuimarisha maendeleo ya wananchi," anafafanua Bashe.

Katika ufunguzi wa mafunzo ya wadadisi wa sensa hii, Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu Dkt. Amina Msengwa, anasisitiza takwimu zina mchango mkubwa katika maandalizi na utekelezaji wa sera na mipango, katika kufanya uamuzi sahihi unaotakiwa.

Anasema sensa ya mwaka wa kilimo 2019/20, ni ya tano kufanyika nchini tangu nchi ipate uhuru.

Meneja Takwimu Ofisi ya Taifa ya Takwimu Mkoa wa Singida, Naing'oya Kipuyo, anaishukuru Serikali kwa kusaidia kufanikisha kazi hiyo, iliyofanyika kwa siku 50.

Kipuyo anasema, taarifa zilizokusanywa kupitia sensa hii kuanzia Oktoba Mosi, 2019 hadi 30 Septemba 30, mwaka jana na kuongeza kuwa, Mkoa wa Singida umekamilisha kazi hiyo.

Anaeleza kwamba, kaya 1,087 zilizochaguliwa katika maeneo madogo 90 ya kuhesabia, zilifikiwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel, anawataka wadau wa uwekezaji kuwekeza katika sekta ya mifugo, watumie fursa ya changamoto ya uhaba wa mbegu za malisho, ambayo mahitaji yake ni zaidi ya tani milioni saba, ambapo uzalishaji wa sasa ni tani 127

Anasema takwimu zinaonesha, kiwango cha uzalishaji wa mbegu ni mdogo ikilinganisha na mahitaji na kwamba, wawekezaji wakigeuza changamoto hiyo kuwa fursa, wataongeza uzalishaji mbegu.

"Mahitaji ya mbegu za malisho Tanzania ni tani milioni saba, lakini kiwango cha mbegu kilichozalishwa kwa mwaka 2019/20 ni tani 127, maana yake kuna uhaba mkubwa, hivyo changamoto hiyo tuitumie kama fursa ya uwekezaji katika sekta hiyo,"anasema Gabriel.

Profesa Ole Gabriel anasema, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo, kampuni na watu binafsi wenye nia ya kuzalisha mbegu bora za malisho.

Katibu Mkuu huyo anasema, lengo ni kufanikisha juhudi za serikali kwa kuleta faida za uchumi, kupitia uwepo wa mifugo nchini na yeye ubora na kwamba suala la malisho bora kwa mifugo lipewe kipaumbele.

"Wananchi wanatakiwa kutumia fursa ya ardhi iliyopo kuzalisha malisho ya biashara, kama wanavyozalisha mazao ya chakula,"anasema Ole Gabriel.

Mabura Makoye ni mfugaji, anasema zipo changamoto nyingi zinazoikabili sekta hiyo, jambo linalochangia kushusha thamani ya mifugo, hivyo serikali inatakiwa kuhakikisha changamoto zote zinatatuliwa.

Scanned with CamScanner

# Wadau wahimizwa upatikanaji taarifa sahihi uvuvi mdogo

Na Mwandishi Wetu, Morogoro

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imesisitiza upatikanaji wa taarifa sahihi za uvuvi mdogo nchini kwa kuangaza taarifa za wavuvi wadogo zilizofichika ili kuweza kutumika kwa mipango ya maendeleo endelevu kwa lengo la kukuza Uchumi.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye hotuba yake ya ufunguzi wa warsha ya wadau wa sekta ya uvuvi ya kupitia matokeo ya utafiti wa mchango wa Uvuvi mdogo iliyosomwa kwa niaba yake na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani (DRTE) Dkt. Erastus Mosha mjini Morogoro mwishoni mwa wiki.

Akisoma hotuba hiyo, Mkurugenzi aliwakumbusha wadau kuwa uvuvi ni sayansi, hivyo usimamizi wa rasilimali hiyo ni muhimu na unahitaji taarifa za kutosha za kitafiti ili kufikia malengo ya kuwa na Uvuvi endelevu nchini.

Alitaja baadhi ya changamoto zinazokabili sekta ya uvuvi kwa muda mrefu kuwa ni kukosekana kwa taarifa sahihi za mavuvi, zana haramu, idadi ya wavuvi, vyombo vya Uvuvi na nyinginezo.

Pia alisema ana matumaini makubwa kuwa matokeo ya utafiti huo wa kuangaza taarifa za uvuvi zilizofichika yatasaidia kuboresha mipango ya sekta ya uvuvi nchini kuendana na kasi ya maendeleo ya viwanda na kuongeza mchango wa sekta kwenye pato la Taifa kutoka asilimia 1.7 hadi asilimia 3.5 ifikapo mwaka 2025.

Aidha katika hotuba yake mgeni rasmi aliwafahamisha wadau kuwa mwaka 2016 Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliingia makubaliano na Shirika la Kilimo na Chakula (FAO) ili kutekeleza mradi wa kuwezesha utekelezaji wa Mwongozo wa Hiari wa Kuhakikisha Uvuvi Mdogo unakuwa Endelevu katika Muktadha wa Uhakika wa Chakula na Kuondoa umasikini.

Aliongeza kuwa matokeo mazuri yanayoendelea kutokea yanatokana na Mradi wa kutekeleza Mwongozo wa Wavuvi Wadogo (SSF Guidelines) ambapo Wizara kwa mara nyingine tena ilisaini makubaliano ya kutekeleza Mradi huo wa kuimarisha mchango wa Uvuvi Mdogo kwa usalama wa Chakula na Maisha Endelevu.

Kwa upande wake kiongozi wa timu ya utafiti Dkt. Paul Onyango kutoka Chuo Kikuu cha Dar es salaam anasema utafiti huo ulifadhiliwa na FAO ulianza Mwaka 2018, na umefanyika kwenye takribani nchi 40 Duniani.

Akigusia matokeo ya utafiti huo, Dkt. Onyango alisema kuwa kuna taarifa nyingi zilizofichika ambazo zinasababisha thamani ya mchango wa uvuvi mdogo kiuchumi kuonekana ndogo sana kitaifa na uhalisia wenyewe.

Dkt. Onyango anabainisha mapendekezo ya kukabiliana na changamoto hiyo kuwa ni vyema Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) kuwa na bajeti maalum ya ukusanyaji takwimu za wavuvi wadogo, kuongeza wakusanya takwimu wenye weledi wa kazi hiyo na pia kutoa elimu kwa wavuvi kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa sahihi kwa Serikali.

Scanned with CamScanner

# Nadau wahimizwa upatikanaji taarifa sahihi uvuvi mdogo

**Na Mwandishi Wetu, Morogoro**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekalia upatikanaji wa taarifa sahihi za uvuvi mdogo nchini kwa kuongeza taarifa za wavuvi wadogo zilizofichika ili [illegible] kutumika kwa mipango ya maendeleo endelevu kwa lengo la kukuza Uchumi.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye hotuba yake ya ufunguzi wa warsha ya wadau wa sekta ya uvuvi ya kupitia matokeo ya utafiti wa mchango wa Uvuvi mdogo iliyosomwa kwa niaba yake na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani (DRTE) Dkt. Erastus Mosha mjini Morogoro mwishoni mwa wiki.

Akisoma hotuba hiyo, Mkurugenzi aliwakumbusha wadau kuwa uvuvi ni sayansi, hivyo utumiaji wa taarifa hiyo ni muhimu na unahitaji taarifa za kutosha za kitafiti ili kufikia malengo ya kuwa na Uvuvi endelevu nchini.

Alitaja baadhi ya changamoto zinazokabili sekta ya uvuvi kwa muda mrefu kuwa ni kukosekana kwa taarifa sahihi za mavuno, zana, maeneo, idadi ya wavuvi, vyombo vya Uvuvi na nyinginezo.

Pia alisema ana matumaini makubwa kuwa matokeo ya utafiti huo wa kuongeza taarifa za uvuvi zilizofichika yatasaidia kuboresha mipango ya sekta ya uvuvi nchini kuendana na kasi ya maendeleo ya viwanda na kuongeza mchango wa sekta kwenye pato la Taifa kutoka asilimia 1.7 hadi asilimia 3.5 ifikapo mwaka 2025.

Aidha katika hotuba yake mgeni rasmi aliwafahamisha wadau kuwa mwaka 2018 Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilisaini makubaliano na Shirika la Kilimo na Chakula (FAO) ili kutekeleza mradi wa kuwezesha utekelezaji wa Mwongozo wa Hiari wa Kuhakikisha Uvuvi Mdogo unakuwa Endelevu katika Muktadha wa Uhakika wa Chakula na Kuondoa umaskini.

Alieleza kuwa matokeo [illegible] yanayoendelea [illegible] mradi [illegible] Mwongozo wa Hiari Wadogo (SSF Guidelines) ambapo Wizara kwa mara nyingine tena itapata makubaliano ya kutekeleza Mradi huo wa kuimarisha mchango wa Uvuvi Mdogo kwa usalama wa Chakula na Maisha Endelevu.

Kwa upande wake kiongozi wa timu ya utafiti Dkt. Paul Onyango kutoka Chuo Kikuu cha Dar es salaam anasema utafiti huo ulifadhiliwa na FAO ulianza Mwaka 2018 na umefanyika kwenye takriban nchi 40 Duniani.

Akitoa matokeo ya utafiti huo, Dkt. Onyango alisema kuwa kuna taarifa nyingi zilizofichika ambazo zinasababisha thamani ya mchango wa uvuvi mdogo [illegible] Uchumi [illegible].

Dkt. Onyango [illegible] changamoto [illegible] Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi [illegible] ya ukusanyaji takwimu [illegible] wavuvi wadogo [illegible] taarifa sahihi kwa Serikali.

Habari Leo Uk.5 Mei 26,2021

# Vichwa vya kuku husaidia utotoleshaji kambale

**Na Lucy Ngowi**

TEKNOLOJIA ya utumiaji wa vichwa vya kuku na bata inasaidia kutotolesha vifaranga vya kambale kwani samaki wa aina hiyo akifugwa hazaliani kama ilivyo kwa yule aliyeko katika mazingira yake halisi, Imebainika.

Mwanafunzi wa mwaka wa tatu anayesomea Elimu ya Ukuzaji Viumbe Hai kwenye maji katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Arnold Shoko, alisema hayo wakati wa Maadhimisho ya Sita ya Wiki ya Utafiti na Ubunifu chuoni hapo mkoani Sar es Salaam.

Alisema kinachofanyika katika teknolojia hiyo ni kupasua kichwa cha kuku au bata ili kutoa 'pituitary gland' itakayotumika kumchoma samaki wa kike na baada ya saa 12 atatoa mayai kisha kurutubishwa na mbegu za kiume.

Alisema baada ya kurutubisha na mbegu za kiume, vifaranga hivyo vya samaki hupatikana baada ya saa 24.

"Samaki aina ya kambale hazaliani kwa hiyo ili azaliane inabidi afanyiwe njia mbadala. Zipo njia nyingi, lakini zina changamoto mbalimbali ikiwepo gharama na matokeo ya mlaji," alisema.

Alisema njia hiyo ya kutumia vichwa vya kuku na bata ni ya bei nafuu na endelevu.

Akifungua maonesho hayo Waziri Mkuu Kassim, alisema amejifunza mambo mengi ikiwemo kuzalisha samaki aina ya kambale ambao katika hali ya kawaida, ukichukua mmoja au wawili hawawezi kuzaa mpaka itumike njia nyingine inayoweza kuzalisha.

"Hayo ni matokeo ya utafiti miongoni mwa niliyoyaona, lakini pia nimekuta ubunifu wa takataka zilizotupwa huko mtaani, mbunifu kachukua kaunganisha katengeneza kapata picha ya mtu kapata viti. Kupitia maonesho haya, mmetupa matumaini makubwa," alisema.

Naibu Makamu Mkuu wa UDSM upande wa Utafiti, Profesa Bernadeta Killian, alisema ili kuendeleza na kuboresha ubunifu na ujasiriamali, mwaka 2016, UDSM ilianzisha kitengo kipya cha ubunifu na ujasiriamali kinachosimamia masuala hayo.

"Pia chuo kimekuwa kikitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wahitimu wa taasisi za elimu ya juu nchini. Kwa mfano, mwaka 2019 tulitoa mafunzo kwa wahitimu takribani 1,600 katika mikoa minane Tanzania," alisema.

Scanned with CamScanner



# Shamba la mifugo lilivyobadilisha maisha ya wananchi Ngerengere

NA MWANDISHI WETU, MOROGORO

KWA kutambua mchango wa sekta ya mifugo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilia-mua kuwekeza katika mashamba ili kuyapa uwezo wa kuzalisha mifugo bora itakayosaidia kuku-za kipato cha taifa na wananchi kwa ujumla.

Ngerengere ni miongoni mwa mashamba matano ya Serikali yaliyo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro mkoani Mo-rogoro.

### HISTORIA YA SHAMBA

Meneja wa Shamba la Seri-kali (LMU) Ngerengere, Saita Ole Kimosa anasema shamba hilo lilianzishwa mwaka 1975 kama shamba la ng'ombe wa maziwa ambalo kabla lilifahamika kama Dairy Farm Company lililokuwa chini ya watu binafsi na baadaye kufilisika na kubadilishwa jina na kuitwa LMU, mwaka 2004 chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Anasema lengo la kuan-zishwa kwa shamba hilo kuwa ni pamoja na kuzalisha mifugo bora yenye tija na kuuziwa wa-nanchi kwa bei ambayo ni rafiki na kujiingizia kipato na kusaidia wananchi kupata mbegu bora za mifugo.

Saita anasema hadi Mei, mwaka huu shamba hilo lilikuwa na mifugo mbalimbali ikiwamo ng'ombe 771, mbuzi 234, nguru-we 201 na limekuwa na uzalishaji mzuri, pia anasema kuwa aina ya mifugo iliyopo kuwa ni ng'ombe aina ya borani, fresian na cho-tara, kwa upande wa mbuzi ana-taja aina ya boa ambayo asili yake ni Afrika ya Kusini na nguruwe aina ya landress na large white.

### MAFANIKIO

Akizungumzia mafanikio ya shamba hilo ambalo lina mifugo takribani 1,206, anasema sham-ba hilo limefanikiwa kuzalisha mifugo mingi na kuisambaza kwa kuwauzia wafugaji wadogo wadogo kwa bei ambayo ni rafiki mikoa ya Morogoro na Dar es Sa-laam.

Anasema shambani hapo kuna mifugo ya aina tatu ikiwa ni ng'ombe, mbuzi na nguruwe ambayo yote inauzwa kwa wa-nachi kwa bei rafiki ili kusaidia wananchi kupata mbegu bora za mifugo.

Kimosa anaendelea kufafan-ua kuwa, kila aina ya mifugo ili-opo shambani hapo kwa kusema, wana ng'ombe aina ya borani, frishian na chotara na kusema kuwa chotara wanapatikana kwa kupandisha borani na freshian na kuongeza kuwa chotara wanao-patikana hapo wana sifa ya kutoa maziwa mengi.

Aidha, kuna mbuzi aina ya bora asili yake ikiwa ni Afrika ya Kusini, ni mbuzi wa nyama na wanafahamika kama mbegu kwa wafugaji na wanaweza ku-pandishwa na mbuzi wa kienyeji na kupata chotara wazuri na wa-naokua haraka sana.

"Pia kuna nguruwe aina ya largewhite na landres ambao wa-nafahamika kwa lengo la kuuzwa kwa wananchi kwa ajili ya mbe-gu bora," anasema Kimosa.

### MCHANGO KWA JAMII

Kwa upande wa mchango, Ki-mosa anasema kuwa wameweza kuwapatia wafugaji mitambo bora kwa bei nafuu, baadhi ya wananchi kupata ajira ndani ya shamba la hilo la serikali, kuwau-zia maziwa wananchi wanaozun-guka shamba hilo pamoja na ku-wapa masai kwa ajili ya kulima.

Pia, wafugaji wananufaika kwa kupata tiba ya mifugo na ushauri kutoka kwa wataalam wa shamba la mifugo la serikali la Ngerengere.

"Wananchi wanahamasishwa kutenga mifugo yao na kufanya uhimilishaji kwa mifugo hiyo pamoja na kuuziwa madume bora ili kuboresha ng'ombe wa asili na kuwauzia chotara.

"Kipindi cha kiangazi kuna lambo linafahamika kama Mkob-ora limetengwa kwa ajili ya wa-nanchi kunyweshea mifugo yao ili kusaidia ng'ombe na mifugo mingine isife kwa kukosa maji maeneo hayo," anasema Kimosa.

### CHANGAMOTO.

Kimosa anabainisha changa-moto ambazo zinakabili shamba hilo ikiwemo miundombinu mi-bovu pamoja uchakavu wa vi-tendea kazi ambavyo hupelekea kushindwa kutimiza baadhi ya majukumu ya kila siku na kutoka eneo moja kwenda lingine kuto-kana na ubovu au kutokuwepo kabisa kwa usafiri.

"Kipindi cha doria wananchi hukasirishwa na wakati mwing-ine kuamua kuchoma moto baa-dhi ya maeneo ya shamba hili, pia kuna uvamizi mdogo sana wa wafugaji kuingiza mifugo na kuli-sha ndani ya shamba na kutoka," anasema Kimosa.

### MIKAKATI

Kwa upande wa mikakati, Kimosa anasema wanatarajia kila mwaka kufanya uzalishaji mkubwa wa mifugo wauze na kupata hela kwa ajili ya kurekebi-sha miundombinu ya shamba na kutatua changamoto zilizo ndani ya uwezo wao.

### WITO KWA WADAU

Kimosa anatoa wito kwa wadau wa mifugo, kwa kusema kuwa mifugo ni rasilimali inay-otoa ajira na ni malighafi ya vi-wanda, hivyo wananchi watumie malighafi hizo vizuri.

"Ni vyema wafugaji kutibu mifugo yao kwa wakati ili kuepu-sha magonjwa yasiyo ya lazima kwa wanyama na kuogesha anga-lau mara moja kwa wiki pamoja na kuchanja kwa wakati.

"Pia wajitahidi kufuga kisasa kisasa na kwa tija kwani mifugo ndio ajira yenyewe, kuchagua mifugo iliyo bora kutunza na kutunza pia ngozi kwani kila kilichopo kwa ng'ombe ni mali pamoja na kuhimilisha mifugo yao ili kupata koo tofauti, na kuepuka kudumaza mifugo kwa kuwa na koo moja inayozunguka kwenye boma.

"Hii husaidia kupata mifugo bora na mizuri zaidi," anasema Kimosa.

Kifuto Kimanga, ni mkazi na mfugaji wa Kiwege, amabaye anasema kwa muda mrefu ame-kuwa akifanya ufugaji wa ku-hamahama ambao ulisababisha yeye na familia yake kutokuwa na makazi maalumu maana kila siku wapo barabarani kutafuta maeneo ya kulishia mifugo yake na wakati mwingine kuingia kwenye migogoro na watumiaji wengine wa ardhi kutokana na mifugo kufanya uharibifu.

"Nimeamua kuachana na adha ya kuhamahama na kuamua kutafuta eneo la kudumu kwa ajili ya makazi na kufanya ufu-gaji wa kisasa ambapo shamba la LMU Ngerengere limenisaidia kupata mbegu bora za mifugo na za kisasa," Kimanga.

Kimanga anasema kuwa uwe-po wa shamba hilo umewasaidia wafugaji kupata mbegu bora za mifugo kama ng'ombe, mbuzi na nguruwe kwa bei nzuri na mifu-go hiyo inakuwa haraka, nyama nyingi na maziwa mengi.

"Kutokana na uwepo wa shamba hili tunapata msaada wa kitabibu kwa mifugo yetu ku-toka kwa wataalam wa mifugo waliopo shambani hapo na elimu juu ya utunzaji bora wa mifugo yetu," anasema Kimanga.

Aidha,Kimanga anaeleza kuwa, mafanikio aliyopata kuto-kana na ufugaji bora na wa kisasa kwani mwaka 2013 ameweza ku-jenga nyumba kubwa ya kisasa yenye uwezo wa kubeba watu 24 inayokidhi haja zao na kuweza kupeleka watoto shule nzuri na za kisasa.

Hata hivyo ameendelea ku-faidika na mifugo hiyo kwani ameweza kuzalisha mbuzi kwaw-ingi na kuiuza kwa bei inayompa faida ambapo hapo awali ali-nunua mbuzi kwenye shamba la LMU Ngerengere kwa bei nafuu sana kwa dume moja alinunua Sh 150,000 na kwa sasa yeye anauza kuanzia Sh 250,000 - 300,000 kwa mbuzi mmoja ambapo anapata faida kubwa na ya kutosha kwa kuendesha maisha yake ya kila siku na kufanya maendeleo.

"Mbuzi hawa ni wakubwa sana, wanakuwa kwa haraka na wana nyama nyingi sana pia ha-wana tofauti na mbuzi wa Tan-zania wa asili zaidi sana ni kuz-ingatia matunzo,chanjo, dawa za minyoo na chakula cha kutosha chenye virutubisho vyote kwa mifugo.

"Kwa upande wa ng'ombe wanatoa maziwa kwa wingi kwa kutoa kuanzia lita 14 kwa siku kila mmoja, pia wana nyama nyingi pindi wanapochinjwa," anasema Kimanga.

Kimanga anaongeza kuwa wanawapa matunzo mazuri kwa kuzingatia kuwachanjo kwa wakati, na kutoa huduma zote za matibabu kwa wakati ili kue-puka kupoteza ng'ombe kwa ma-gonjwa yasiyo ya lazima.

Pia, Esther Kilinga mfugaji wa Kiwenge jirani na shamba la LMU Ngerengere, anasema namna al-ivyonufaika, ambapo ameweza kujipatia madume kutoka sham-bani hapo na kwa sasa ana jumla ya ng'ombe 200 na kutokana na mifugo hiyo amefanikiwa kujen-ga nyumba ya kisasa ya kuishi, nyumba za wageni (gesti) zina-zowaingizia kipato na kuweza kuendesha maisha yao ya kila siku.

"Pia tumeweza kujenga kani-sa na kuwasomesha watoto kwe-nye shule nzuri na za kisasa.

"Lakini pia nauza maziwa, samli na mifugo iliyo hai kwa wa-nakijiji wa Ngerengere na maeneo jirani na hii hupelekea kunufaika na ufugaji wangu na kuweza ku-changia pato la Taifa," anasema Esther.

Aidha, mfugaji mdogo, Athumani Ramadhani anasema kuwa alianza ufugaji mwaka 2018 akiwa na ng'ombe watatu na kufika sasa amefikisha ng'ombe 10 na kuainisha faida alizozipata kutokana na ngombe hao kuwa ni pamoja na kujenga nyumba ya kisasa, kukidhi mahitaji ya familia yake ambapo awali hali ilikuwa mbaya.

Aidha, Athumani anashuk-uru uwepo wa shamba la LMU Ngerengere kwani limeweza ku-wasaidia wafugaji wengi kupata mbegu bora za mifugo inayowa-saidia kuzalisha kwa wingi na ku-fundishwa kanuni za ufugaji bora na tiba kwa mifugo yao na ku-weza kupata lita nane za maziwa kwa ng'ombe mmoja kwa siku.

"Ombi langu kwa Serikali itu-saidie kutujengea josho wafugaji wa majumbani kwani kwa ku-tumia solo kwa ng'ombe wengi ni kazi ngumu kidogo, kwani pia dawa haiwafikii vizuri na wakati mwingine mifugo mingine huk-wepa dawa hivyo kutofanikisha lengo la kuogesha.

"Pia nawashauri wafugaji wengine kutumia vizuri shamba la LMU Ngerengere kwani lipo kwa ajili yao na watapata mifu-go bora na mizuri sana inayotoa maziwa lita nane kwa siku kwani kama tunavyotambua kuwa ng'ombe ni mali," anasema

# Minister instructs SUA to invent simple technology

**By Guardian Correspondent, Morogoro**

LIVESTOCK and Fisheries Minister Mashimba Ndaki has instructed the Sokoine University of Agriculture (SUA) in Morogoro Region to research on and invent simple low cost technology to help farmers to abandon the hand hoe in order increase crops production.

He said in doing so, they will have honoured in deeds the late Edward Moringe Sokoine who fought for SUA's establishment to increase farmers' and livestock keepers economic wellbeing by using the raw materials they produce.

Ndaki made the remarks in his opening speech for the 17th SUA Commemoration for the late Edward Sokoine who was the country's Prime Minister, being 37 years since his death in 1984.

He said the use of modern technology in agriculture and livestock keeping has many benefits including production of sufficient food and increase farmers and herders' incomes thereby contributing to the reduction of poverty.

He said statistics show that 64 per cent of farmers in the country still use the hand hoe with negligible benefits compared to those using modern machinery.

He said the agricultural sector was still an important foundation of Tanzania's economy just as it is for many other countries that depend on agriculture since it will continue to provide significant contribution to the economy for many years to come.

In regard to the livestock sector, Ndaki said as a country, Tanzania has not performed well as the Livestock Sector's Vision for 2016/201 to 20231/2032 has shown that the country produced only 3 billion litres of milk.

He said out of that quantity 2.1 billion litres or 70 per cent was from traditionally kept cows and the rest from modern kept cows.

All in all, he said the utilization of farming technology, profitable production and competition for products and agricultural services have great potential to push forward the wheel of the country's development.

The Guardian Uk.2 Mei 26,2021

Scanned with CamScanner



## KUTOKA ZANZIBAR

NA EMMANUEL MOHAMED

**Sh. bilioni 84.1>>** Fedha zilizoidhinishwa Wizara ya Biashara na

# Ujenzi kiwanda cha kusarifu dagaa, kuongeza thamani mwani wanukia

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema mchakato wa kuanzisha viwanda viwili muhimu vya kusarifu samaki aina ya dagaa na kuongeza thamani ya zao la mwani, unatarajiwa kuanza kipindi cha mwaka wa fedha 2021-2022.

Imesema viwanda hivyo ni mkombozi kwa wafanyabiashara wadogo na wazalishaji wa kilimo cha mwani ambao kwa asilimia 80 wanawake.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, aliyasema hayo jana, alipokuwa akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2012-2022.

Alisema malengo na mikakati ya serikali ya awamu ya nane chini ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kimarisha sekta ya viwanda, hatua ambayo itasaidia kuongeza mapato na ajira kwa vijana.

Shaaban, alisema mradi huo unaotarajiwa kutekelezwa na sekta binafsi ukiwemo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na Taasisi ya Kilimo ya TAHA utatekelezwa Fungurefu, Mkoa wa Kaskazini Unguja na Mkokotoni Unguja.

Alisema yamekuwepo mafanikio makubwa katika uzalishaji wa dagaa eneo la Fungurefu, ambao wamepata umaarufu mkubwa na soko lake kuimarika.

Waziri huyo alisema tayari samaki hao wanaozalishwa Fungurefu, Mkokotoni, Unguja, soko lake la uhakika lipo nchi za Afrika ya Mashariki hadi Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (Congo DRC).

Alisema tayari mpango wa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya zao la mwani unaendelea huko Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba na wapo hatua za kukamilisha ramani na makisio ya kununua vifaa vya ujenzi zinazofanywa kwa ushirikiano na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), kampuni ya Ocean Fresh na Kappa Carrageenan Nusantara kutoka Indonesia.

Aliwataka wakulima wa mwani Unguja na Pemba kuongeza kasi ya uzalishaji wa kilimo hicho kwa lengo la kukidhi mahitaji na matarajio ya kiwanda.

Mbali na hilo, Waziri Shaaban alisema serikali itanunua zao la karafuu kwa mujibu wa bei iliyopo katika soko la dunia, kwa kuwa hushuka na kupanda, hivyo Shirika la Taifa la Biashara halitanunua tena karafuu kwa bei ya sh.14,000 kwa kilo ambayo ni ya zamani.

Wajumbe wa baraza hilo, walipitisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021-2022 na kuidhinisha sh. bilioni 84.1 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

Scanned with CamScanner





# Viwanda vya dagaa, mwani kuanzishwa

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

MCHAKATO wa kuanzishwa viwanda viwili vya kusarifu samaki aina ya dagaa pamoja na kuongeza thamani ya zao la mwani unatarajiwa kuanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021-2022.

Viwanda hivyo vinatajwa kuwa ni mkombozi kwa wafanyabiashara wadogo pamoja na wazalishaji wa kilimo cha mwani ambao kwa asilimia 80 ni wanawake.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shaaban, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2012-2022 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani.

Alisema malengo na mikakati ya serikali ni kuimarisha sekta ya viwanda hatua ambayo itasaidia kuongeza mapato pamoja na ajira kwa vijana.

Shaaban alisema mradi huo unatarajiwa kutekelezwa na sekta binafsi ikiwamo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) pamoja na Taasisi ya Kilimo (TAHA), unatarajiwa kutekelezwa huko Fungurefu na Mkokotoni, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema yamekuwapo mafanikio makubwa katika uzalishaji wa samaki aina ya dagaa eneo la Fungurefu na samaki hao wakipata umaarufu mkubwa na soko lake kuimarika.

"Tayari samaki aina ya dagaa wanaozalishwa Fungurefu Mkokotoni, Unguja soko lake la uhakika lipo katika nchi za Afrika ya Mashariki hadi Jamhuri ya Kidemokrasia ya (Congo DRC)," alisema.

"Mheshimiwa Spika mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kuimarisha sekta ya viwanda vya aina mbalimbali ikiwamo vidogo ambavyo vitaongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kuingia katika masoko," alisema.

Alisema, ujenzi wa kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya zao la mwani kinaendelea huko Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema ujenzi wa kiwanda unaendelea ukiwa katika hatua za kukamilisha ramani na makisio ya kununua vifaa vya ujenzi ambao unafanywa kwa ushirikiano na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), pamoja na kampuni ya Ocean Fresh na Kappa Carrageenan Nusantara kutoka Indonesia.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha kilo 240 za bidhaa ya dagaa na kinatarajiwa kuzalisha mwani na kusarifu jumla ya tani 30,000 kwa mwaka.

Aliwataka wakulima wa mwani Unguja na Pemba kuongeza kasi ya uzalishaji wa kilimo hicho kwa lengo la kukidhi mahitaji na matarajio ya kiwanda.

Scanned with CamScanner

# Wastani wa maziwa watajwa kuwa lita 237 kwa mwaka

**Na LATIFA GANZEL,** Morogoro

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema wastani wa maziwa yanayozalishwa na ng'ombe mmoja kwa mwaka ni lita 237.

Amesema kiasi hicho ni kidogo ukilinganisha na uzalishaji wa maziwa kwa ng'ombe wa Amerika.

Waziri Ndaki aliyasema hayo jana mjini Morogoro katika ufunguzi wa maadhimisho ya kumbukizi ya aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward yanayofanyika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA).

"Nchi ya Marekani ambayo ni namba moja kwa uzalishaji maziwa, ng'ombe anatoa wastani wa lita 10,503 kwa mwaka," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2019/2020, Tanzania ilizalisha lita bilioni 3.0 za maziwa kati ya hizo, lita bilioni 2.1 zilitokana na ng'ombe wa asili na lita bilioni 0.9, zilitokana na ng'ombe wa kisasa.

"Hii ni kwa sababu tuna ng'ombe wa maziwa wachache, kati ya ng'ombe milioni 33.4 waliopo nchini, wa maziwa ni milioni 1.95 sawa na asilimia 5.8 tu," alisema waziri huyo.

Alieleza kama nchi kupitia SUA ikishirikiana na taasisi pamoja na wadau wengine wa mifugo nchini, itazalisha teknolojia zaidi ili kuboresha uzalishaji wa maziwa nchini.

Alisema kutokana na nchi kuwa na fursa bora za viwanda vinavyoweza kutumia malighafi za mazao kilimo, mifugo na uvuvi katika kuendeleza uchumi wake, ni muhimu kuondokana na dhana ya kufanya kilimo, mifugo na uvuvi kwa mazoea.

"Nawasa Watanzania waendelee kulima, kufuga kisasa na kibiashara ili kuwasaidia kuinua vipato vyao kama sehmu ya kuenzi maono ya Hayati Sokoine kwa vitendo," alisema.

Alisema miongoni mwa mambo aliyoyasimamia kwa umahiri na umakini mkubwa hayati Sokone ni nchi kujitosheleza kwa chakula, kusimamia uwekezaji mkubwa katika sekta ya kilimo na mifugo na kutoa msisitizo wa kulima na kufuga kisasa na kwa tija.

"Moja ya maono yake kwa nchi, ilikuwa ni kuanzisha mikoa maalumu ya kuzalisha chakula kinachoweza kutosheleza mahitaji ya nchi nzima," alisema.

Pia, alisema hayati Sokoine ni miongoni mwa wazalendo wakubwa ambae nchi imewah kuwa nae.

Alitumia muda wake mwingi kujitoa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania na nchi kwa ujumla.

"Tukiwa tumetimiza miaka 37 tangu tumpoteze mzalendo huyo katika kumkumbuka kwetu, tuna kila sababu ya kuyakumbuka na kuyaenzi mawazo na matendo yake ambayo yamechangia kuimarisha misingi ya maendeleo ya nchi yetu," alisema.

Alisema ni vizuri kumuenzi hayati Sokoine kwa kuwahimiza watafiti wa SUA na taasisi zingine kuendelea kubuni na kuzalisha teknolojia ambazo zitachangia kuboresha kilimo, mifugo, uvuvi, maliasili na sayansi shirikishi.

Pia, kuzisambaza kwa jamii ili ziweze kutumika kuongeza tija katika uzalishaji.

Alisema takwimu zinaonyesha sekta ya kilimo huchangia takribani asilimia 70 ya ajira, asilimia 30 ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi huku asilimia 65 ya malighafi za viwandani.

Alisema asilimia 64 ya wakulima nchini, hutumia jembe la mkono, asilimia 24 hutumia wanyamakazi na 12 hutumia matrekta.

"Upande wa sekta ya mifugo, kama nchi bado hatujafanya vizuri kwani kwa mujibu wa uchambuzi wa mwelekeo wa mifugo Tanzania," alieleza.

Awali, Makamu Mkuu wa SUA, Profesa Rafael Chibunda, alisema wanafanya juhudi za kuongeza shughuli za chuo maeneo tofauti nchini lengo likiwa kusogeza huduma karibu na wananchi.

Maeneo hayo ni Morogoro, Arusha, Katavi, Ruvuma, Tanga, Iringa na Njombe.

Alisema katika nyanja ya utafiti, SUA ilishika nafasi ya kwanza nchini kwa kupata nukuu 89,752.

"Katika kutekeleza majukumu yake, chuo chetu jukumu lake kuu limekuwa kufanya utafiti kwa mafanikio kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo."

Uhuru uk.16 Mei 26,2021

Scanned with CamScanner